**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA AFYA**

MKOA WA SINGIDA
Anuani:"AFYA

Simu Na: 026-2502397
Fax Na: 026-2502360
E.mail: regionalhospital@singida.go.tz
Unapojibu tafadhali taja:

HOSPITALI YA RUFAA MKOA
S.L.P. 104,

SINGIDA.

**Kumb. MB.329/377/01/12** **25/08/2025**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KUJITOLEA

Kaimu Mganga Mfawidhi Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Singida anawatangazia Watanzania wenye sifa kuomba nafasi za kujitolea katika kada ya Udereva na Utunzaji kumbukumbu(Mapokezi).

### 1.0 DEREVA DARAJA LA II-NAFASI 2

**1.1 Majukumu ya kazi ya Dereva Daraja la II**

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
iii. Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari.
iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
vi. Kufanya usafi wa gari.
vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake wa kazi.

**1.2 SIFA ZA MWOMBAJI**

i. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha VETA au NIT au chuo kingine kinachotambuliwa na serikali.
ii. Awe na leseni ya udereva daraja C au E.
iii. Awe na cheti cha ufaulu wa mtihani wa kidato cha IV.
iv. Mwombaji mwenye cheti cha majaribio ya ufundi atafikiriwa kwanza.
v. Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
vi. Mwenye uzoefu wa kazi atapewa kipaumbele.

### 2.0 MAPOKEZI(RECEPTIONIST)-NAFASI 4

**2.1 Majukumu yake:**

i. Kupokea wateja na kuingiza taarifa kwenye mfumo kwa ajili ya kuonana na daktari.
ii. Kuelekeza wateja mahali pa kupatiwa matibabu.
iii. Kutunza kumbukubu za wateja kupitia mfumo wa matibabu.
iv. Kutoa maelekezo sahihi kwa wateja juu ya taratibu za kulipia matibabu na kuingiza kwenye mfumo.
v. Kutunza fomu za Bima ya afya na kuziwasilisha kwa wakati Kitengo cha bima.
vi. Kutunza kumbukumbu za wagonjwa na kuhakikisha zinapatikana kwa wakati zinapohitajika.

vii. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu uzoefu na ujuzi wake.

## 2.2 Sifa za mwombaji

i. Waombaji lazima wawe wahitimu wenye Astashahada katika fani ya Utunzaji wa Kumbukumbu kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.
ii. Awe na Elimu ya kidato cha nne.
iii. Awe na umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45.
iv. Awe raia wa Tanzania na ambaye hajawai kushtakiwa kwa makosa ya jinai.
v. Mwenye uzoefu wa kazi na uwezo wa kutumia kompyuta atapewa kipaumbele.

## 2.3 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI

i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na mwenye umri usiopungua miaka 18 na usiozidi miaka 45;
ii. Kila mwombaji anatakiwa aambatishe nakala ya vyeti vya Elimu ya Sekondari na taalumavinavyohitajika kulingana na Kada husika kama ilivyofafanuliwa katika tangazo hili;
iii. Kila Mwombaji aambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa;
iv. Uwasilishaji wa vyeti vya kugushi utapelekea kuchukuliwa hatua za kisheria;
v. Mwombaji aambatanishe Wasifu binafsi (CV) akionesha uzoefu, namba za simu, anuani yake na anuani za wadhamini watatu (3) wa uhakika.
vi. Mwombaji aambatishe picha ndogo (Passport size) mbili (2) kwenye barua ya maombi;
vii. Mwombaji aambatanishe nakala ya Kitambulisho cha NIDA au namba ya NIDA.
viii. Waombaji watakaokidhi vigezo wataitwa kwenye usaili na watakaoshindwa kuzingatia masharti ya Tangazo hili hawataitwa
ix. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **30.08.2025 saa 9:30 Alasiri**.
x. Aidha atakaewasilisha barua yake kwa njia ya mkono ahakikishe anasaini kitabu maalumu cha kupokea barua hizi masijala.
xi. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kingereza
xii. Maombi yote yatumwe au yawasilishwe **ofisi ya Masjala ya wazi** au kupitia barua pepe; **barua@sigidarrh.go.tz** kwa anuani ifuatayo: -

**Mganga Mfawidhi,**
**Hospitali ya Rufaa Mkoa wa Singida,**
**S.L.P 104,**
**SINGIDA.**

*Dkt. David J. Mwasota*
**Kaimu Mganga Mfawidhi**
**Hospitali ya Rufaa Mkoa**
**SINGIDA**

MEDICAL OFFICER IN CHARGE
SINGIDA REGIONAL REFERRAL HOSPITAL
P. O. Box 104
SINGIDA